
# IWE NURU

## UJUMBE WA BIBLIA WA KUENEZA INJILI



# IWE NURU

Waandishi: Paula Kilpatrick and Joan Carter

Masomo ya Mikutano ya Wanawake

Africa Coordinated Curriculum for Women

Co-Lit 2-2-1

Published and Printed by
Baptist Publications House
Box 30370, Thika Road, Nairobi

© Copyright, 1990

Baptist Publications House

All rights reserved

shamba hili na anawafundisha wakulima jinsi ya kupanda mazao mengi. Kuna mradi wa ngano, kuku, na wa ng'ombe. Waamini hukutanika pale shambani kwa Ibada na kujifunza Biblia.

**SEHEMU YA TANO:** Ushuhuda wa Vijana

Zambia ina makundi ya kushuhudia ya vijana ambao huwafundisha Wakristo wapya. Makundi ya vijana watano watano hufundisha jinsi ya kushuhudia. Hujifunza pia jinsi ya kuwafundisha waamini wapya kuhusu maisha ya Kikristo na kanisa.

Kisha vijana hawa hutumwa sehemu mbalimbali. Kundi moja la watu thelathini na tano walitembelea vijiji saba. Waliwapata Wakristo wapya 330 baada ya wiki tatu. Walifundishwa jinsi ya kuwa wanafunzi na wakawa tayari kuanzisha makanisa mapya.

**KIONGOZI**

Kuna uhuru wa kuhubiri nchini Zambia. Wazambia na wamisheni, wazee kwa vijana, wanaume kwa wanawake, wote wanashirikiana pamoja. Wanahubiri na kufundisha. Bible Way Correspondence School, Redio, Muziki, Vijikaratasi vya kusoma, na hata shamba vinasaidia kuwaleta watu kwa Bwana. Makanisa mengi yanahitajika. Tuwaombee Wazambia wanapotafuta kuanzisha makanisa nchini mwao.

**MAOMBI**

Je! umepata njia mpya za kushuhudia kutoka kwa mpango wa leo?



# YALIYOMO

## UJUMBE WA KUENEZA INJILI KATIKA BIBLIA

Mwandishi: Bi. Paula Kirkpatrick

1. Mpango Wake Mungu
2. Mungu Akimchagua Ibrahimu
3. Musa Anawaongoza Watu wa Mungu
4. Watu Wengine Waliomfuata Mungu
5. Manabii Wakilifunua Kusudi la Mungu.
6. Ahadi za Mungu Zikitimizwa na Yesu
7. Yesu na Wayahudi
8. Yesu na Watu Wasio Wayahudi
9. Kufa na Kufufuka kwa Yesu
10. Mafundisho ya Mwisho ya Yesu
11. Roho Mtakatifu Hutoa Nguvu za Kuweza Kushuhudia
12. Zambia: Tayari kwa Ushuhuda

Co-Lit 2-2-1

kumwamini Yesu. Kweli Mungu amesikia maombi!

Nchi zipatazo ishirini na moja za Afrika zina Bible Way Correspondence Schools.

Kijana mmoja aitwaye Wesley Chiromo, alisoma vitabu vyake vyote. Alianza kuwashuhudia watu wengine. Mwishowe alimwandikia na kumwomba Mmisheni mmoja aje kuwabatiza watu kumi na saba waliokuwa wameamini. Hili ndilo lililokuwa kanisa la kwanza kuanzishwa na mwanafunzi wa Bible Way. Makanisa mengine yalifuatia baadaye.

SEHEMU YA TATU: Kufundisha

Musa Chimfumpa hakumfuata Mungu kwa muda wa miaka arobaini. Lakini sasa ni kiongozi wa Kibatisti. Je! kwa nini alibadilika?

Wazazi wa Musa walikuwa Wakristo. Baba yake alikuwa mzee wa kanisa. Alijifunza Biblia alipokuwa angali mdogo. Lakini aliacha mambo ya dini alipoondoka nyumbani.

Alifanya kazi ya kutoza ushuru chini ya serikali ya wakoloni. Aliwapiga watu na kuwafunga gerezani walipokataa kulipa kodi. Aliweza kujibu maswali ya Biblia kwa hivyo kila mtu alifikiria kuwa ni Mkristo.

Baadaye alifanya kazi ya udaktari. Alipofanya kazi hii aliona tofauti kubwa kati ya Wakristo na wasio Wakristo. Wakristo walikufa wakiwa na furaha. Wasio Wakristo waliogopa sana kifo. Baba yake Mkristo alikufa bila kuwa na hofu yo yote. Jambo hili lilimfanya Musa aanze kufikiria tena Ukristo.

Alianza tena kusoma Biblia yake. Mwishowe aliamua kwenda, yeye na mkewe kwenye mkutano wa uinjilisti. Kisha akakiri imani yake katika Yesu Kristo.

Alianza mara moja kumtumikia Bwana. Alianza kufundisha Biblia nyumbani kwake. Alifundisha Shule ya Jumapili na hata akahubiri.

Alianza kujifunza katika seminari ya Kibatisti ya Zimbabwe alipotimia umri wa miaka 43. Baadaye alifanya kazi ya uchungaji na kuanzisha makanisa mengi mapya baada ya kuhitimu. Baadaye pia, alifanya kazi na Bible Way, akijibu maswali yaliyoulizwa na wanafunzi. Hatimaye alianza kufundisha pale chuoni. Alifanywa mwalimu mkuu wa hapo mnamo mwaka wa 1986.

Mafundisho ambayo Musa alijifunza yalimwezesha kuwashuhudia wengine. Anawafundisha wengine sasa hivi ili kukuza ushuhuda.

SEHEMU YA NNE: Ukulima

Wamisheni wa Kibatisti wa Zambia walipewa shamba lenye hekari 2,088. Shamba hili lilianzishwa na Daktari Moffat, aliyekuwa jamaa ya David Livingstone. Jamaa hii iliwapatia Wabatisti shamba hili wakati Daktari Moffat alipokufa. Waliwataka walitumie kwa kuwasaidia Wazambia na kuhubiri Injili. Wabatisti wanafurahia kufanya kazi hii.

Mmisheni mmoja anaishi katika

wachungaji wa Zambia wanatumainia kuwaambia habari njema watu wapatao milioni 7.1 wa Zambia kwa kushirikiana pamoja. Makanisa yanaombwa kufanya mkataba wa "kuagana na kushirikiana." Wamekubaliana kutoa kiasi fulani cha pesa kutoka kwa sadaka zao kutegemeza Wamisheni wanne wa Jumuia Kuu na maprofesa wawili wa seminari ambao ni wananchi wa Zambia. Wanatarajia kulipa asili mia ya mishahara hii ni miradi mingine yote ifikapo mwaka wa 1994.

Hitaji kubwa lililoko Zambia ni kwa makanisa mengi kuwashuhudia watu ambao wako tayari kusikiliza. Wamisheni wametambua sehemu kumi pale Lusaka ambazo zinahitaji makanisa. Je! ni nani atayaaanzisha? Itawabidi kuwepo Wamisheni wengi au wahubiri wa Kizambia waliohitimu. Hitaji hili litatimizwa kwa kushirikiana pamoja kulipa mishahara ya wafanya kazi hawa.

Njia nyingi zinatumiwa kuwaambia watu ujumbe wa Injili. Wabatisti wa Zambia hutayarisha na kutangaza redioni vipindi vipatavyo mia nne kwa mwaka katika lugha nne tofauti. Vipindi hivi hutangazwa na shirika la utangazaji la Zambia. Vingine hutangazwa na Trans World Radio.

Baptist Publications huchapisha vitabu vinavyotumiwa na Shule ya Jumapili na Ushirika wa Wanawake. Huchapisha maelfu ya vijikaratasi vya mafundisho ya Biblia katika lugha nyingi tofauti.

Mashindano ya nyimbo huwafanya watu wengi kutaka kumjua Yesu Kristo.

Wanawake Wabatisti wa Zambia hufanya kazi pamoja na washiriki wengine wa makanisa katika mpango wa uinjilisti na kuwafundisha wanafunzi. Wanawake Wabatisti wa Zambia huvaa mavazi rasmi ya rangi ya zambarau na nyeupe. Ni lazima mwanamke ajifunze na ajue vifungu fulani vya Biblia ndipo avae vazi hili. Hii huwasaidia kuwa mashahidi wema.

**SEHEMU YA PILI:** Kutumia Biblia

Mmisheni mmoja wa Zambia aitwaye Tom Small, aliandika kitabu kiitwacho "Yesu Yu Nani?" mnamo miaka ishirini na tano iliyopita. Aliomba kwamba mtu mmoja tu asome kitabu hicho na amwamini Yesu kama Mwokozi.

Wakati huo kulikuwepo na Wamisheni watano na wake zao kule Zambia. Hapakuwepo na makanisa mengi, wala wachungaji. Wamisheni hawa waliamua kwamba wataweza kuwaambia watu wengine habari za Yesu kama watakuwa na masomo ya Biblia kwa njia ya posta.

Vitabu vingine tisa vimeandikwa tangu wakati huo na vinatumiwa na Bible Way Correspondence School (Masomo ya Biblia kwa Njia ya Posta). Vitabu hivi vinachapishwa katika lugha ya Kiingereza, Chichewa, Bemba na Kaonde. Wanafunzi wapatao elfu mia moja na hamsini walijiandikisha katika Bible Way Correspondence School ya Zambia katika mwaka wa 1986. Wanafunzi wapya hujiandikisha kila mwezi na





## MPANGO WAKE MUNGU

**Kiini cha Mwezi:** Ujumbe wa Kueneza Injili katika Biblia

**Maandiko ya Ibada Fupi:** Waefeso 3:1-13

**Kifungu cha Kukumbuka:**

"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi." Warumi 5:8

### KIONGOZI WA MPANGO

"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi" (Mwanzo 1:1). Kifungu cha kwanza cha Biblia hujibu swali la maana sana linaloulizwa na watu wengi. Watu wengi huuliza, "Ni nani aliyeviumba vitu hivi?" Biblia inasema ya kuwa, "Mungu ndiye aliyeziumba mbingu na nchi." Sehemu hiyo nyingine ya Biblia inatueleza sababu ya Mungu kuumba ulimwengu huu.

Mungu analo kusudi katika kila jambo aliolitenda. Ikiwa utajifunza Biblia unaweza kujifunza kusudi lake ni nini kwako wewe na kwa watu wote.

**SEHEMU YA KWANZA:** Haja ya Kuwa na Mpango

Sura kumi na moja za kwanza za kitabu cha Mwanzo zinaeleza habari za kuumbwa kwa ulimwengu na hata kuumbwa kwa mwanadamu. Mungu alimwumba mwanadamu ili ashirikiane na Mungu. Mwanadamu alipovunja ushirika wake na Mungu, basi naye Mungu alitengeneza mpango wa kumpatanisha mwanadamu na Mungu tena. Biblia inatueleza vile Mungu alivyoufunua mpango wake kwa mwanadamu. Zamani za Agano la Kale Mungu aliufunua mpango wake kwa kuwatumia manabii na watu wengine waliokuwa watawa. Katika Agano Jipya Mungu alifunua mpango wake kwa njia ya Mwanaye, Yesu Kristo.

**SEHEMU YA PILI:** Mpango Ulifunuliwa

Yesu alipokuja ulimwenguni akiwa na mwili wa mwanadamu, alimfunulia mwanadamu mpango wa Mungu ulio kamili. Daima mpango wa Mungu kwa mwanadamu ulikuwa mwema. Yesu alipokuja akafa msalabani kwa ajili ya dhambi za mwanadamu, alionyesha jinsi pendo lake lilivyo kuu kwa mwanadamu. "Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu. Tulipokuwa tungali wenye dhambi" (Warumi 5:8).

**SEHEMU YA TATU:** Mpango Ulishirikishwa

Yesu alipokufa msalabani, alifufuka kutoka katika wafu, na alipaa kwenda mbinguni, kila kitu kilichohitajika kumleta mtu ili ashirikiane na Mungu

kilikuwa kimekwisha timia. Kazi yote ya kuuleta wokovu ilikuwa imekwisha fanywa. Sasa mwanadamu aliweza kumwamini Mungu na halafu aweze kuupata wokovu. Sasa watu wote wanaweza kumwendea Mungu.

Mungu hakupanga mwanadamu ampokee Kristo tu kama Mwokozi wake. Lakini ulikuwa mpango wake pia kwamba wale wanaomwamini Yesu kama Mwokozi wao waushirikishe mpango huu wa wokovu kwa watu wote.

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Biblia inatuambia ya kuwa Mungu anao mpango kwa ajili ya kila mtu. Mpango huo unamkubali kila mtu ashirikiane naye kwa njia ya Mwanaye Yesu Kristo aliyesema, "Mimi ndimi njia na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6).

**WAKATI WA KUSHIRIKI:**

Waulize wanawake watatu washuhudie vile Mungu alivyoyabariki maisha yao tangu walipoongoka. Kila mmoja anaweza kuchukua muda wa dakika tano tu.

**Mpango wa Pili**

## MUNGU AKIMCHAGUA IBRAHIMU

**Kiini cha Mwezi:** Ujumbe wa Kueneza Injili Katika Biblia

**Maandiko ya Ibada Fupi:** Matendo 7:2-8

**Kifungu cha Kukumbuka:**

"Akamwamini Bwana, naye akamhesabia jambo hili kwa haki." Mwanzo 15:6

**KIONGOZI**

Sura kumi na moja zinazotangulia katika kitabu cha Mwanzo hutuambia ya kuwa mwanadamu alizidi kuwa mwovu baada ya dhambi kuingia hapa ulimwenguni. Wakati fulani kulikuwa na mtu mmoja aliyekuwa mtawa katika dunia. Naye mtu huyo aliitwa Nuhu. Mungu aliviangamiza viumbe vyote vya ulimwengu isipokuwa Nuhu na jamaa yake pamoja na wanyama wale aliowaingiza katika safina; lakini baada ya gharika jamaa ya Nuhu waliendelea kuishi katika dhambi.

Mungu alifahamu ya kuwa kulikuwa na njia moja tu ya kushinda dhambi ili ndipo mwanadamu apate kupatanishwa na Mungu tena.

**SEHEMU YA KWANZA:** Ahadi kwa Ibrahimu

Mungu alianzisha mpango wake kwa kumchagua Ibrahimu. Mungu hakumchagua Ibrahimu kwa sababu alimpenda yeye zaidi ya watu wengine waliokuwa duniani. Ibrahimu hakuchaguliwa kwa sababu alikuwa mtu wa haki kama Nuhu. Biblia haituelezi ni kwa nini Mungu



barabara ya kwenda Dameski, mtume Paulo alikuwa mtu wa maana sana katika uipeleka Injili kwa watu wa Mataifa. Katika maono Paulo alimwona mtu wa Makedonia akimwambia aenende katika nchi yake akawapelekee habari njema. Kabla ya kifo chake kule Rumi, Paulo aliyaanzisha makanisa mengi yenye Wayahudi na watu wa mataifa ambao waliamini.

Kwa muda wa miaka mingi Roho Mtakatifu aliendelea kuwaongoza watu kuipeleka habari njema ya Yesu kwa watu wote. Watu wengi

wamekwisha sikia habari njema kwa sababu Roho Mtakatifu alinena na Wakristo hao akawatuma kama alivyomtuma mtume Paulo katika sehemu ambazo habari njema haijapelekwa.

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Kusudi la Mungu halijabadilika bado. Hata sasa ni kusudi la Mungu watu wote wa dunia wamjue Yeye kuwa ndiye Mungu mmoja wa kweli. Tangu wakati ule Yesu alipokuwa hapa ulimwenguni, wateule wa Mungu wa kutimiza ahadi hii mpya ni watu wale waitwao Wakristo. Kila mmoja wetu aliyempokea Yesu Kristo ndani ya moyo na maisha yake anao wajibu ulio sawa na ule uliopewa wana wa Ibrahimu. Kila mtu anapaswa kumtii Mungu. Kila mtu anaweza kuwa baraka kwa watu wale wengine anapowapeleka kwa Yesu.

**Mpango wa Kumi wa Mbili**

**ZAMBIA: TAYARI KWA USHUHUDA**

**KIINI CHA SOMO:** UMISHENI

**MAANDIKO MATAKATIFU:** Matendo 28

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:** "Akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu." Matendo 28:31

**KIONGOZI**

Mtume Paulo alikuwa huru kuhubiri alipokuwa gerezani. Aliweza kuwashuhudia wafungwa wengine na wageni hata ingawa alikuwa amefungwa. Kifungu chetu cha kukumbuka kimetuelezea jambo hili. Kisome tena.

Kifungu hiki kinaelezea pia ushuhuda wa Wabatisti wa Zambia. Wachungaji na Wamisheni wako huru kuhubiri na kufundisha. Tujifunze sasa jinsi wanavyotekeleza kazi hii.

**SEHEMU YA KWANZA:** Kushirikiana Pamoja

Wabatisti na Wamisheni

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Yesu aliwaagiza wafuasi wake kungojea kule Yerusalemu mpaka watakapopokea nguvu ile waliyoihitaji katika kushuhudia. Wanafunzi walikuwa wamekutana pamoja wakiomba wakati wa siku kuu ya Pentekoste. Wakati ule Roho Mtakatifu aliwajilia na kuwapa wanafunzi nguvu.

Baada ya wanafunzi kupokea nguvu za Roho Mtakatifu, walikuwa tayari kuutimiza mpango wa Mungu wa kuwaleta watu wote wa dunia kwa yeye. Wafuasi wa Yesu walikuwa wamekwisha ona ufunuo kamili wake Mungu ndani ya Yesu. Kazi ya Masihi ilitimizwa. Kwa sababu ya nguvu za Roho Mtakatifu sasa, kundi lile ndogo linaweza kupeleka Habari Njema kwa watu wote wa ulimwengu.

**SEHEMU YA KWANZA:** : Wayahudi Walisikia Wakati wa Pentekoste. Mojawapo ya ishara za kuonyesha kujiliwa kwa wanafunzi na Roho Mtakatifu wakati wa sikukuu ya Pentekoste ni ile ya uwezo wa wanafunzi kunena kwa lugha kumi na tano mbalimbali. Walishuhudia katika lugha ya kila mtu aliyekuwa amehudhuria sikukuu ya Pentekoste.

Wakati Petro alipowahubiria watu, kila mtu aliyesikia hotuba yake aliweza kuifahamu. Katika siku hiyo ya Pentekoste watu wapatao 3,000 walimkiri Yesu.

**SEHEMU YA PILI:** Watu wa Mataifa Wamesikia Habari Njema

Kornelio alikuwa akida wa Kirumi. Hakuwa Myahudi. Alikuwa mtu amchaye Mungu. Wakati alipozungumza na Kornelio, alitii magizo ya Mungu na alimtuma mtu aende akamwite Petro.

Wakati Mungu alipoongea na Petro katika maono, Petro hakuyafahamu mafundisho yake Mungu. Ujumbe wa Mungu ulikuwa na tofauti na ule ambao Petro alikuwa amekwisha fundishwa tangu utoto wake. Petro alipofahamu hakika ya vile Mungu alivyokuwa akitaka afanye, aliyafuata maagizo yake Mungu.

Baada ya Petro kuihubiria nyumba ya Kornelio watu wote wa nyumba yake walimwamini Yesu kama Mwokozi na Bwana wao. Petro alifahamu zaidi habari za ujumbe wake Mungu. "Petro akafumbua kinywa chake, akasema, 'Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo; bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye'" (Matendo 10:34-35). Petro aliendelea kuzipeleka habari njema kwa Wayahudi na kwa watu wa Mataifa.

**SEHEMU YA TATU:** Ulimwengu Wote Kusikia Habari Njema

Roho Mtakatifu aliwaongoza Wakristo wa kwanza kuenenda ulimwenguni mwote. Wakristo walipotembea ulimwengu wote, waliwaambia habari za Yesu na habari za kifo na kufufuka kwake. Nao watu wengi waliamini. Nao hao wenye kuamini walikaa wakiwa waaminifu kwa Yesu wakati wa mateso.

Baada ya kumwona Yesu katika



alimchagua Ibrahimu. Mungu alimwambia Ibrahimu atende jambo fulani kisha akampa Ibrahimu ahadi. Naye Ibrahimu alimwamini Mungu. Naye Mungu aliweza kumtumia Ibrahimu katika mpango wake kwa sababu alimwamini.

Katika Mwanzo 12:1-3 hutueleza vile Mungu alivyomwambia Ibrahimu. Mungu alimwambia Ibrahimu aondoke nchi yake aende mpaka nchi ambayo Mungu atamwambia. Mungu alimwambia, "Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa."

**SEHEMU YA PILI:** Ahadi kwa Isaka

Mungu alijaribu imani ya Ibrahimu alipomwamuru amtoe mwanaye pekee kuwa sadaka ya kuteketeza. Ibrahimu alipotafuta njia ya kumtii Mungu, naye Mungua alimpa sadaka nyingine kutoa kuwa dhabihu. Katika Waebrania 11:19 Maandiko Matakatifu yanasema ya kuwa Ibrahimi alimwamini Mungu sana hata akaamini kama Isaka angekufa Mungu angemfufua.

Ibrahimu alimwambia Isaka vile Mungu alivyomfunulia. Baada ya kutoa dhabihu Mungu alimkumbusha Ibrahimu ahadi ile tena. Lakini wakati Isaka alipokuwa akawa mtu mzima, Mungu mwenyewe aliirudia ahadi ile tena kwake Isaka. (Usome Mwanzo 26:2-5).

**SEHEMU YA TATU:** Ahadi Kwa Yakobo

Isaka aliwazaa Yakobo na Esau wakiwa pacha. Mungu alimchagua mwana aliyekuwa mdogo, yaani Yakobo, kuwa yule atakayetekeleza ahadi ile. Maana ya jina Yakobo ni kusema "Mjanja." Esau aliuza haki ya mzaliwa wa kwanza ili apate chakula cha tumbo. Halafu Yakobo alimdanganya Esau akamnyang'anya haki ya mzaliwa wa kwanza. Yakobo alitaka sana kubarikiwa katika maisha, lakini hakufahamu njia za kuzipata baraka hizo. Mungu aliona kuwa kulikuwa na kitu katika maisha ya Yakobo ambacho aliweza kukitumia.

Yakobo alipotoroka kutoka kwa ndugu yake Esau, Mungu alinena na Yakobo katika ndoto. Basi Yakobo alianza kujifunza kutoka kwake Mungu. Kwanza alijifunza ya kuwa Mungu hakuwa Mungu wa Isaka peke yake. Alijifunza ya kuwa Mungu alikuwa Mungu wa watu wote. Mungu alianza kumbadilisha Yakobo kuwa mtu ambaye angaliweza kumtumia. Baada ya miaka mingi Mungu alilibadilisha jina la Yakobo kuwa Israeli, yaani, "anayeshindana na Mungu" (Mwanzo 35:10).

**SEHEMU YA NNE:** Mwanamke Mwafrika Aliyeamini

Wakati mwingine hata siku za leo Mungu huongea na mtu fulani. Mwanamke mmoja mzee wa nchi ya Nigeria ambaye ni Mkristo mwaminifu sana alisimulia vile mmisheni mmoja alivyowasili kwao alipokuwa mtoto mdogo. Hapo mbeleni alikuwa hajawaona wazungu. Hakujua habari za Yesu wala hakufahamu mengi kuhusu Mungu. Mmisheni aliwauliza watoto wote kama wanataka kuhudhuria shule. Alikuwa ndiye

mtoto pekee aliyekubali kuhudhuria. Wengine wote waliogopa. Aliacha wazazi na watu wa nyumba yao akaenda bila kujua kule alikokwenda. Baada ya kukaa shuleni mwaka mmoja alimwamini Yesu kama Mwokozi wake. Tangu wakati huo alimtumikia Yesu akiwa kama mwalimu, mke wa mchungaji na kama mtenda kazi ya Ushirika wa Wanawake. Anaamini kuwa Mungu alinena naye akamwambia aende shule hata wakati ule alipokuwa mtoto mdogo asiyeweza kuyafahamu mambo. Alitii na baadaye akiwa shuleni alijifunza habari za Yesu na habari za kusudi la Mungu katika maisha yake.

**KIONGOZI WA MPANGO**

Ibrahimu, Isaka na Yakobo walikuwa watu wa imani. Walimwamini Mungu na walijifunza kumtii Yeye. Nguvu za kumwezesha kuziona ahadi za Mungu hutegemea utii wake.

**Mpango wa Tatu**

## MUSA ANAWAONGOZA WATU WA MUNGU

**Kiini cha Mwezi:** Ujumbe wa Kueneza Injili Katika Biblia

**Maandiko ya Ibada Fupi:** Matendo 7:17-34

**Kifungu cha Kukumbuka:**

"Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa." -Waebrania 11:1, 2

**KIONGOZI WA MPANGO**

Katika miaka ile ambayo wana wa Israeli waliishi katika nchi ya Misri, sehemu ya kwanza ya ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu ilikuwa dhahiri. Vizazi vya Ibrahimu vilizidi kuongezeka sana hata Farao mfalme wa Misri alianza kuwaogopa wana wa Israeli. Ingawa walikuwa chini ya adhabu kali ya utumwa, Wana wa Israeli walizidi kuongezeka na kuwa na nguvu nyingi. Halafu Mungu alimchagua mtu aliyeitwa Musa awaongoze wana wa Israeli kwenda katika Nchi ya Ahadi na kulianzisha taifa mpya.

**SEHEMU YA KWANZA:**Utiifu

Miezi mitatu baada ya wana wa Israeli kutoka katika nchi ya Misri, Mungu alinena nao katika mlima wa Sinai. Kwanza, Mungu alinena na Musa. Na katika kitabu cha Kutoka 19:5-6, Mungu anamwamuru Musa kuwaambia wana wa Israeli kuwa wakizitii amri zake, watakuwa watu wake walio wateule kati ya mataifa yote ya dunia. Nao watakuwa taifa la ukuhani na takatifu kwake Mungu. Wana wa Israeli waliyakubali mapatano haya.

**SEHEMU YA PILI:** Ahadi kwa Taifa



Yesu aliwatuma wanafunzi wake ulimwenguni wakiwa na kazi ya kufanya. Aliwatuma kuipeleka injili yake yenye toba na wokovu katika ulimwengu wote. Hapa tena amewapa nguvu za Roho Mtakatifu ili awaongoze wanapoitenda kazi yake.

Katika Yohana 21:15-17 Yesu alikuwa akizungumza na Petro kuhusu wajibu wake katika Ufalme wa Mungu. Alimwuliza Petro mara tatu kama anampenda Yesu. Naye Petro alijibu mara tatu kwamba anampenda. Yesu alimwambia katika kila jibu kwamba, "Lisha kondoo wangu." Yesu alikuwa akimwambia Petro kwamba awatunze wale watu ambao Yesu alikufa ili ndipo awaokoe. Katika kifungu cha 19 Yesu alimwambia Petro, "Nifuate." Vile Yesu alivyomwambia Petro humwambia kila mwenye kuamini.

**SEHEMU YA TATU:** Amri Kuu

Amri Kuu ya Yesu imeandikwa zaidi ya mara moja katika Injili. Kifungu kimoja cha maana kinachojulikana sana hupatikana katika Mathayo 28:16-20. (Visome vifungu hvii kutoka katika Biblia yako.) Yesu alinena na wanafunzi wake faraghani katika nchi ya Galilaya. Aliwaambia wanafunzi wake kuupeleka ujumbe wake kila mahali waendapo. Hakuwapa amri peke yake ya kuenenda ulimwenguni mwote, bali aliwaahidi kuwa atakuwa pamoja nao kila mahali waendapo.

**KIONGOZI WA MPANGO**

Katika kila sehemu ya Maandiko Matakatifu Yesu anawaambia wanafunzi wake kwamba wao ndio watakaoupeleka ujumbe wake wa wokovu katika ulimwengu wote. Pia anawaambia ya kuwa hawatakuwa peke yao. Anasema ya kuwa atakuwa pamoja nao wanapoenda kutoka sehemu moja kwenda nyingine na kuwaambia habari za Yesu.

**Mpango wa Kumi na Moja**

## ROHO MTAKATIFU HUTOA NGUVU ZA KUWEZA KUSHUHUDIA

**Kiini cha Mwezi:** Ujumbe wa Kueneza Injili Katika Biblia

**Maandiko ya Ibada Fupi:** Matendo 2:1-21, 38, 39

**Kifungu cha Kukumbuka:**

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." Matendo 1:8

Mpango wa Kumi

# MAFUNDISHO YA MWISHO YA YESU

**Kiini cha Mwezi:** Ujumbe wa Kueneza Injili Katika Biblia

**Maandiko ya Ibada Fupi:** Matendo 1:1-11

**Kifungu cha Kukumbuka:**

"Basi Yesu akawaambia tena, Amani iwe kwenu; kama Bwana alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi." Yohana 20:21

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Baada ya Yesu kufufuka kutoka katika wafu, alijidhihirisha kwa wanafunzi wake mara nyingi katika muda wa siku arobaini kabla ya kupaa kwake kwenda mbinguni. Yesu alipozungumza na wanafunzi wake aliwaambia tena vile alitaka wafanye. Yesu aliwakumbusha wanafunzi wake karibu safari tano baada ya kufufuka kwake ya kwamba watakuwa mashahidi wake katika ulimwengu wote.

**SEHEMU YA KWANZA:** Unabii Wake Mungu Umetimia

(Soma Katika Biblia Yako Luka 24:44-49). Jioni ya siku ile aliyofufuka, Yesu aliwatokea wanafunzi wake kumi pamoja na wale waliokuwa wamekutana pamoja nao. Yesu aliwaambia ya kuwa unabii wa Agano la Kale ulikuwa umekwisha timizwa. Unabii huo ulipatikana katika torati ya Musa katika unabii na Zaburi. Basi hapo ndipo walipoanza kufahamu kabisa juu ya kazi ya Yesu akiwa kama Masihi. Katika Luka 24:25 husema ya kuwa Yesu alifungua akili za wanafunzi wakaanza kufahamu Maandiko Matakatifu yaliyonenwa naye. Katika vifungu 46 na 47 Yesu amesema kwa ufupi yale yote yaliyonenwa habari zake katika Maandiko. Yesu alisema, "Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu."

Baadaye Yesu aliwachagua wafuasi wake kuwa ndio watakaoupeleka ujumbe wake kuhusu msamaha wa dhambi katika ulimwengu wote. Yesu alifahamu ya kuwa wanafunzi wake hawawezi kufanya kazi hiyo kwa nguvu zao wenyewe. Aliwaahidi kutuma Roho Mtakatifu ili awape nguvu za kuwawezesha kuupeleka ujumbe wake ulimwenguni mwote.

**SEHEMU YA PILI:** Yesu Kawatokea Wafuasi Wake

Yohana aliandika habari za kujidhihirisha kwa Yesu ambako alijidhihirisha mara nyingi kwa wanfunzi wake. Safari mbili za kujidhirisha kwake kunapatikana katika Yohana 20:19-23 na Yohana 21-15-17. (Soma vifungu hivi kutoka katika Biblia yako.)

Katika Yohana 20:19-23 Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi."



Mungu alinena na wana wa Israeli katika mlima wa Sinai na aliwapa zile Amri Kumi. Kuzisikia amri zile kumi hakuwazuia wana wa Israeli kuivunja amri ya kwanza baada ya majuma matatu.

Mungu alipowaona wana wa Israeli wakiabudu ndama wa shaba alighadhabika sana. Katika kitabu cha Kutoka 32:7-8 Mungu huwaita wana wa Israeli watu "wako" badala ya watu "wake". Wana wa Israeli walikuwa wamemwasi Mungu. Hawakuweza kuendelea kuwa watu wake.

**SEHEMU YA TATU:** Kukataa Mungu

Hadithi ya watu wa Israeli inahuzunisha sana. Watu wa taifa hili walikataa mara kwa mara kumwamini Mungu. Tena Mungu alipowaambia wana wa Israeli kuingia katika Nchi ya Ahadi, walikataa kuingia. Mungu aliwaambia kuwa amewapa nchi ile. Kile ambacho walihitaji kufanya ni kuingia katika nchi hiyo, lakini watu walikataa kumwamini Mungu.

Katika kitabu cha Hesabu sura ya 14, Musa alimsihi Mungu asiwaangamize watu baada ya watu hao kukataa na kumdharau Mungu na Musa. Mungu alijibu maombi ya Musa akaliokoa taifa, lakini Mungu aliwakataza watu waliotenda dhambi kuingia katika nchi ya ahadi. Nao watu walizunguka jangwani kwa muda wa miaka arobaini mpaka Mungu alipoinua kizazi kipya ambacho kiliweza kumwamini yeye.

**SEHEMU YA NNE:** Kusudi la Mungu

Je, unafahamu kusudi la Mungu katika maisha yako? Wakristo wengi siku hizi hufikiri ya kuwa wao hutimiza kusudi la Mungu ikiwa wamejiunga na kanisa. Watu wengine wanafikiri kuwa wanaweza kununua wokovu kwa njia ya kutoa pesa nyingi. Nao wengine hawajafikiri ya kuwa Mungu analo jambo analotaka wafanye.

Mungu analo kusudi kwa maisha ya kila mtu. Kwanza, anataka kila Mkristo kuzaa matunda. Tunda la Mkristo ni kumzaa Mkristo mwingine. Ikiwa tunataka kuzaa matunda kwa ajili yake, ni lazima tuombe na kusoma Biblia zetu ili ndipo tuweze kujua vile itupasavyo kumtii Mungu. Halafu tunaweza kutoka nje na kuwaambia wengine habari za Mwokozi kwa sababu tunayo hakika kwamba Roho wake atatutangulia.

**KIONGOZI WA MPANGO**

Wana wa Israeli hawakuweza kufahamu Mungu alitaka wawe watu wa aina gani. Kile tu walichojua ni kwamba walikuwa wakimwabudu Mungu wa kweli na yule aishiye. Hawakuweza kufahamu kwamba Mungu alitaka watu wote wamwabudu yeye. Walidhani kuwa Mungu alikuwa wao peke yao. Hawakumtii Mungu ili aweze kuwatumia kuwasaidia watu wengine duniani wajifunze kumwabudu yeye. Hawakuwa taifa la ukuhani wa kifalme.

Mpango wa Nne

## WATU WENGINE WALIOMFUATA MUNGU

**Kilni cha Mwezi:** Ujumbe wa Kueneza Injili Katika Biblia

**Maandiko ya Ibada Fupi:** Zaburi 67

**Kifungu cha Kukumbuka:**

"Basi, mpendeni mgeni, kwa sababu ninyi wenyewe mlikuwa wageni katika nchi ya Misri." Kumbukumbu la Torati 10:19

**KIONGOZI WA MPANGO**

Agano la Kale linatuambia habari za watu ambao hawakuwa Waisraeli ambao walijifunza kumwabudu Mungu. Wana wa Israeli waliambiwa na Mungu wawe wakiwapenda wageni. Watu wa mataifa wangalikubaliwa kuwa Wayahudi iwapo wangalimwamini Mungu. Katika nyakati mbali mbali za historia ya watu wa Mungu, watu wasio Wayahudi walikubali kumwabudu Mungu.

**SEHEMU YA KWANZA: Wale Waliochagua Kumfuata Mungu wa Kweli**

Yethro alikuwa mkwewe Musa. Alikuwa Mmidiani. Naye Yethro aliitengeneza madhabahu ya kumwabudu Mungu. Aliamini kuwa Mungu ndiye aliyekuwa Mungu wa kweli. Musa alimkaribisha Hobabu, mwana wa Yethro, aandamane na wana wa Israeli na azishiriki baraka za Mungu pamoja nao.

Katika kitabu cha Hesabu sura ya 22 tunaambiwa habari za Balaamu. Yeye hakuwa Mwebrania, lakini alikuwa nabii wa Mungu. Wakati wana wa Israeli walipoanza kupigana vita nao wakashinda wakaingia katika Nchi ya Ahadi, walisaidiwa na mwanamke aliyeitwa Rahabu. Mwanamke huyo alikubali kuwa Yehova ndiye Mungu wake wa kweli nao Waisraeli walimkubali pamoja na jamaa yake.

**SEHEMU YA PILI: Ruth Yule Mmoabu**

Hadithi ya Ruthu inadhihirisha kuwa Mungu alikuwa na kusudi watu wengine washiriki katika Mpango Wake wa kuwaleta watu wote wa Mungu mwenyewe.

Ruthu alikuwa mwanamke kijana aliyeishi katika nchi ya Moabu. Baada ya kifo cha mumewe, Ruthu alichagua kuambatana na Naomi, mkwewe, alipokata shauri kurudi katika nchi ya Kanaani. Wakati Naomi alipomwambia Ruthu arudi akarejee nyumbani kwa mamaye, Ruthu alijibu, "Usinisihi nikuache, nirejee nisifuatane nawe; maana wewe uendako nitakwenda, na wewe ukaapo nitakaa. Watu wako watakuwa watu wangu, na Mungu wako atakuwa Mungu wangu" (Ruthu 1:16).



mwana kondoo badala ya kumtoa Isaka, alimtoa mwnaye Yesu awe sadaka kwa ajili ya watu wote.

**SEHEMU YA PILI: Sadaka Yake Mwenyewe Juu ya Msalaba**

Yesu aliyatoa maisha yake msalabani kwa sababu hakuna njia nyingine ya watu wote kuupata wokovu. Yesu alijaribiwa kama mtu mwingine awaye yote. Aliteswa kwa majaribu na aliyashinda alipokufa hapo msalabani.

Tunakuwa warithi pamoja na Yesu kwa sababu alipouawa alitufanya kuwa wenye haki. Alitupatanisha na Mungu kwa sababu ya haki yake. Sisi tuna mahali katika Ufalme wa Mungu kwa sababu Yesu alikufa kwa ajili yetu.

**SEHEMU YA TATU: Mungu Huyarudisha Maisha**

Katika siku ya tatu Mungu alimfufua Yesu kutoka katika wafu. Yesu alimtii Mungu. Aliamini kuwa Mungu angalimfufua kutoka katika wafu. Nguvu za dhambi na mauti zilishindwa wakati Mungu alipomfufua Yesu kutoka katika wafu. Sasa woga na makosa zinaweza kuondolewa kutoka katika maisha ya mtu.

Tumaini letu hupatikana katika uaminifu wa Yesu Kristo. Vile Mungu alivyomtendea Yesu, vivyo hivyo huwatendea watu wote wanaomwamini na kumtii yeye. Mungu alimfufua Yesu katika wafu ili aweze kuthibitisha imani yetu.

**SEHEMU YA NNE: Maisha Mapya kwa Mfungwa**

Mara kwa mara Wakristo huwasahau wafungwa walioko gerezani. Lakini mchezaji mashuhuri wa mpira wa nchi ya Amerika aitwaye Bill Glass hakuwasahau hao wafungwa. Alipokuwa mchezaji wa mpira aliweza kuwashuhudia wachezaji wenzake. Alipoacha kucheza mpira, alianza kazi ya kuwahubiria wafungwa kila siku. Zaidi ya wafungwa 1000 pamoja na walinzi wa gereza wamekwisha pokea maisha mapya katika Kristo kwa sababu ya kazi yake.

Wengi wa watu hao ni wale walioupenda mchezo wa mpira. Kwa hivyo kila siku alikuwa akiwapelekea katika uwanja wa mpira kuwafundisha jinsi ya kucheza vema. Halafu baada ya mpira walihudhuria kanisa ndogo alipokuwa akitoa mahubiri yake.

Yesu Kristo alishinda dhambi na kifo. Hata wauaji na wezi wanaweza kushinda hayo hukumu ya makosa ya dhambi zao kwa kumwamini Yesu.

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Historia moja ya maana sana ulimwenguni ni hiyo ya kufa na kufufuka kwake Yesu msalabani. Yesu alitimiza yote ambayo mwanadamu hawezi kujitendea yeye mwenyewe. Wakati Mungu alipomfufua Yesu kutoka katika wafu, aliweza kumwezesha kila mtu awe na sehemu katika mpango wake Mungu.

wa Samaria pale kisimani, kwa sababu alikuwa amekwisha kuwaambia wanafunzi wake kwamba anataka kupitia nchi ya Samaria. Yule mwanamke wa Samaria pamoja na wanafunzi wa Yesu walishangazwa na yale Yesu aliyofanya. Yesu alikuwa amekwisha vunja kanuni nyingi za desturi za Kiyahudi kwa sababu ya kuongea na Mwanamke wa Samaria.

Yesu alimwambia yule mwanamke ya kuwa saa inakuja, nayo sasa ipo ambayo waabuduo halisi watamwabudu Mungu kwa roho na kweli. Naye Yesu alimwambia huyo mwanamke Msamaria kuwa mimi ninayesema nawe ndiye Masihi aliyeahidiwa na manabii.

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake na hata siku hizi anafundisha kwa vielelezo vya maisha yake. Hufundisha kwa vitu vile alivyovifanya. Aliwafundisha wanafunzi wake na aliwatuma kwenda kuwa mashahidi. Kwanza walitumwa kwenda kwa watu wao halafu walitumwa kwenda kwa watu wote.

**Mpango wa Tisa**

## KUFA NA KUFUFUKA KWA YESU

**Kiini cha Mwezi:** Ujumbe wa Kueneza Injili

**Maandiko ya Ibada Fupi:** Marko 15:21-39

**Kifungu cha Kukumbuka:**

"Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi."

Yohana 14:6

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Neno "Kristo" kwa lugha ya Kiyunani ndilo "Masihi" kwa lugha ya Kiebrania. Jina "Masihi" na "Kristo" huwa na maana ya kusema yule aliyepakwa mafuta. Makuhani, manabii na wafalme walipakwa mafuta. Yesu alikuwa kuhani, nabii na mfalme. Pia alikuwa Mwana Kondoo wa Mungu wa kuzitwaa dhambi za ulimwengu.

**SEHEMU YA KWANZA:** Yesu, Ndiye Sadaka Pekee ya Kutosha

Yesu alisema kuwa, "Ibrahimu aliiona siku yangu" (Yohana 8:56). Kutimizwa kwa ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu kuliwezekana kwa sababu alikufa msalabani. Yesu alikuwa ndiye sadaka ya Mungu. Yesu alikuwa sadaka pekee ambayo Mungu aliweza kuikubali.

Yesu hakutenda dhambi. Hakustahili kufa. Alikuwa Mungu halisi. Lakini Yesu alijinyenyekeza mwenyewe na kama wanadamu alimtii Mungu. Yesu alijua ya kuwa mapenzi ya Mungu yalikuwa afe pale msalabani ili watu wote wawe na nafasi ya kushirikiana na Mungu. Kama vile Mungu alimpatia Ibrahimu sadaka ya



Baadaye Ruthu aliolewa na mtu mmoja aitwaye Boazi wa jamaa ya Naomi. Nao walikuwa vizazi vya mbari ya mfalme Daudi. Ruthu alikuwa ukoo wa uzazi wa Yesu, aliye Masihi.

**SEHEMU YA TATU:** Naamani Yule Mshami

Naamani alikuwa Jemadari wa jeshi la mfalme mwenye nguvu sana wa nchi iliyokuwa upande wa Kaskazini mwa nchi ya Israeli. Mjakazi mmoja alitekwa akawa mtumwa wa mke wa Naamani. Wakati yule msichana alipojua kwamba Naamani alikuwa na ukoma, alimwambia mke wa Naamani habari za Elisha nabii wa Mungu aliyekuwa katika nchi ya Israeli.

Naamani alienda mpaka nchi ya Israeli na aliweza kuponywa kwa nguvu zake Mungu. Alipoponywa alisema ya kuwa, "Tazama, najua ya kwamba hakuna Mungu duniani mwote, ila katika Israeli." Naamani aliahidi kuwa hataabudu sanamu au miungu wa uongo hata kidogo.

**SEHEMU YA NNE:** Ndugu Mhindi

Chama cha Baptist World Alliance ni mwungano wa Wabatisti wote kutoka katika nchi zote za ulimwengu. Wao huchapisha gazeti ambalo huenda kusomwa katika sehemu nyingi za dunia. Gazeti moja lilitumwa katika kanisa moja la Wahindi wa kabila la Naga linaloishi upande wa kaskazini mwa nchi ya India.

Walishangaa walipojua ya kwamba kuna Wabatisti wengi ulimwenguni. Mkulima mmoja alisema ya kuwa, "Lo, ni ajabu! Ni ajabu kusema ya kuwa hapo mbeleni nalikuwa nikiamini kwamba Wabatisti ni watu wa kabila la Naga na watu wengine wa Kiamerika peke yao. Sasa nimekwisha fahamu ya kuwa Wakristo Wabatisti wako kila mahali ulimwenguni."

Ni kusudi la Mungu kwamba injili ya Yesu Kristo iwafikie watu wa mataifa na wa kila kabila. Ni kusudi lake kwamba Wakristo waupeleke ujumbe huu wa Wokovu.

**KIONGOZI WA MPANGO**

Kitabu cha Zaburi ni mkusanyiko wa nyimbo zilizoimbwa katika ibada ya kumwabudu Mungu. Kusudi la Mungu la kumpatanisha mwanadamu na yeye mwenyewe ndicho kiini cha Zaburi nyingi. Zaburi ya 67 ni mwito kwa Wayahudi wampeleke Mungu kwa mataifa yote ya ulimwengu. Katika maisha ya watu wa kabila la Kiyahudi hawakupenda kutekeleza ujumbe wa wimbo huu. Kwa hivyo Agano la Kale huwa na hadithi chache tu za watu wengine waliokubali kumwabudu Mungu wa kweli. Lakini kusudi la Mungu limetendeka katika maisha ya watu hao.

# YESU NA WAYAHUDI

**Kiini cha Mwezi:** Ujumbe wa Kueneza Injili Katika Biblia

**Maandiko ya Ibada Fupi:** Isaya 11:1-10

**Kifungu cha Kukumbuka:**

"Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa Bwana, kama maji yaifunikavyo bahari."
Habakuki 2:14

**KIONGOZI WA MPANGO**

Manabii wa Agano la Kale waliongea na wana wa Israeli kuhusu dhambi zilizokuwa katika maisha ya watu. Nao hao manabii waliwaalika watu kwenye toba. Amosi ndiye nabii aliyeonyesha haki na hukumu ya Mungu kwa sababu ya maovu yaliyokuwa katika maisha ya watu wa Israeli.

Nabii katika ujumbe wao pia waliwakumbusha watu kusudi alilowakusudia alipowachagua. Nabii Hosea aliufahamu upendo wa Mungu kwa watu wote wa ulimwengu. Maandishi ya manabii hueleza habari za hukumu ile ambayo ingaliwapata wana wa Israeli wangalikataa kuwaambia watu wa mataifa mengine habari za Mungu yule aishiye.

**SEHEMU YA KWANZA:** Isaya

Unabii wa Isaya hueleza habari za kuja kwa Masihi na vile kusudi la Mungu litatimizwa. Maandishi ya Isaya yanaeleza mengi kuhusu vile mambo yatakavyotukia kuliko nabii mwingine awaye yote. Pia Isaya anawaonya wana wa Israeli. Mungu alikuwa amejifunua zaidi kwa wana wa Israeli kuliko kwa mataifa mengine. Kwa sababu ya jambo hili wana wa Israeli walikuwa na hukumu kuu kuliko watu wengine.

Tena Isaya aliwakumbusha watu wa Mungu ya kuwa wanastahili kuwa mashahidi kwa watu wote wa ulimwengu wa kupinga wasiabudu sanamu. Isaya alikaza walipaswa kuwa nuru kwa watu wa mataifa. Manabii wote walijua ya kuwa Yehova alikuwa ndiye Mungu wa mataifa yote. Katika Isaya 66 nabii Isaya ameona maono ya wakati ambao mataifa yote watamwabudu Mungu.

**SEHEMU YA PILI:** Yona

Mungu alimwita Yona kwenda kuhubiri katika mji wa Ninawi. Wakati Yona alipojaribu kutoroka kutoka katika uso wake Mungu, alijifunza ya kuwa Yehova alikuwa ndiye Mungu wa ulimwengu wote. Yona hakufurahi wakati watu wa Ninawi walipotubu na kuanza kumwabudu Mungu.

Yona ni mfano wa wana wa Israeli. Wana wa Israeli walikumbushwa juu ya kusudi lile ambalo Mungu alikuwa nalo kwa ajili yao. Hawakuufurahia mpango wa Mungu. Hawakutaka Mungu awabariki watu wengine wa





# YESU NA WATU WASIO WAYAHUDI

**Kiini cha Mwezi:** Ujumbe wa Kueneza Injili Katika Biblia

**Maandiko ya Ibada Fupi:** Yohana 12:20-32

**Kifungu cha Kukumbuka:**

"Kwa maana hakuna tofauti ya Myahudi na Myunani; maana yeye yule ni Bwana wa wote, mwenye utajiri kwa wote wamwitao; kwa kuwa kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka."
Warumi 10:12-13

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Yesu alikuwa akihubiri kwa wana wa Israeli. Wanafunzi wake aliwatuma kwanza kwenda kuhubiri kwa wana wa Israeli. Ilikuwa nafasi yao ya mwisho ya kutimiza ahadi hiyo. Biblia inaeleza katika sehemu nyingi vile Yesu alivyofanya alipokutana na watu ambao sio Wayahudi.

**SEHEMU YA KWANZA:** Yesu na Mwanamke Mkananayo

Yesu alinena na mwanamke mmoja aliyetaka Yesu amponye binti yake. (Soma Mathayo 15:22-28). Kwanza, Yesu aliijaribu imani yake kwa kutomjali. Nao wanafunzi wake walimwomba Yesu amkubali aende zake kwa sababu alikuwa akiwasumbua kwa kuomba omba. Halafu Yesu akajaribu imani yake kwa kusema ya kuwa wokovu ulikuwa kwa ajili ya Wayahudi. Wakati mwanamke alipokuja na kumsihi tena, Yesu alisema ya kuwa, "Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa." Mwanamke alikubali jambo hilo kwa kusema, hata mbwa hula makombo yaangukayo kutoka mezani pa bwana zao. Yesu alipoona vile imani ya huyo mwanamke ilivyo kuu, aliikubali dua yake. Naye binti yake aliponywa.

**SEHEMU YA PILI:** Yesu na Akida wa Kirumi

(Soma Kutoka Katika Mathayo 8:4-13). Yesu alikuwa katika Kapernaumu wakati akida huyu wa Kirumi alipomwomba Yesu aje amponye mtumishi wake aliyekuwa mgonjwa sana. Yesu alipokubali kwenda pamoja na mtu huyo, yule akida alisema ya kuwa, "Bwana, mimi sistahili wewe uingie chini ya dari yangu. Lakini kama ukisema neno tu, mtumishi wangu atapona."

Yesu alishangazwa na imani ya huyo mtu, naye Yesu aliwaambia makutano ya watu kuwa watu wengi wasio Wayahudi kama akida huyo, kutoka sehemu nyingi za dunia wataketi pamoja na Ibrahimu, Isaka na Yakobo katika ufalme wa mbinguni.

**SEHEMU YA TATU:** Yesu na Mwanamke wa Samaria

(Soma Kutoka Biblia Yako Yohana 4:7-26). Yesu alipopitia nchi ya Samaria alizungumza na mwanamke

walikataa kumsaidia mwenzao. Mgeni yule aliyechukiwa na Wayahudi ndiye aliyemsaidia yule mwenye kujeruhiwa. Yesu alisema ya kuwa tuenende tukawe kama huyo Msamaria. Yesu alisema ya kuwa mtu anaweza kufahamu kama unazishika amri za Mungu kwa yale unayotenda lakini si kwa yale unayoamini na kuyasema.

**SEHEMU YA PILI: Mungu Huwatafuta Wale Waliopotea**

(Soma Kutoka Biblia Yako: Luka 15:3-32). Katika Luka 15 Yesu anasimulia hadithi za kuonyesha vile upendo wa Mungu ulivyo kwa wale walio mbali naye. Hadithi hizi husimulia habari za shilingi, kondoo aliyepotea, na habari za yule mwana mpotevu. Huonyesha ya kuwa Mungu huwatafuta wale ambao hawamjui. Mungu huwatafuta wale waliopotea na huwa na furaha mmoja akipatikana.

Katika hadithi ya mwana mpotevu, baba anasimama mahali pa Mungu. Naye ndugu yule wa kwanza anasimama mahali pa Israeli. Mwana huyo mkubwa amekasirika kwa sababu yule mwana aliyepotea amerudi nyumbani. Hataki ashirikishwe baraka za babaye. Hataki kushiriki na ndugu yake aliyekuwa akiishi dhambini na kuishi mbali na Mungu. Baba amefurahi kwa sababu mwanaye aliyekuwa amepotea amerudi nyumbani. Mungu anamkumbusha yule mwanawe wa kwanza ya kwamba anazo baraka zote za babaye. Mungu anamwambia mwanawe wa kwanza ajiunge pamoja naye kwa sababu mwanaye aliyekuwa amepotea amerudi nyumbani.

**SEHEMU YA TATU: Karamu Kubwa**

(Soma Kutoka Biblia Yako: Luka 14:16-24). Katika Injili ya Luka sura ya 14 Yesu alisimulia hadithi ya mtu mmoja ambaye alifanya karamu na aliwakaribisha wageni wengi. Wakati wa kula chakula ulipofika, alimtuma mtumwa wake aende awaambie wale walioalikwa waje karamuni. Wote walioalikwa walitoa udhuru wa kutofika. Mwenye nyumba aliposikia hivyo alikasirika na akamwambia mtumwa wake aende katika njia kuu na vichochoro vya mji, akawalete maskini, vilema, vipofu na viwete. Yule Bwana aliposikia kuwa kungali na nafasi, alimtuma mtumishi wake aende nje barabarani na mipakani kuwaleta watu waingie ili nyumba yake ipate kujaa. Naye Bwana alisema, "Maana nawaambia ya kwamba katika wale walioalikwa, hapana hata mmoja atakayeionja karamu yangu."

Katika hadithi hii yule bwana ni Mungu na wale walioalikwa walikuwa ni Wayahudi.

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Viongozi wengi wa dini hawakuamini ya kuwa Yesu alikuwa ndiye Masihi. Walikuwa wakitazamia Masihi ambaye ataweza kuwafanya huru kutoka katika utawala wa Warumi. Walishindwa na kufahamu vile Yesu alikuwa akitaka kusema. Yesu alipowakemea kwa sababu ya kutoamini kwao, viongozi wa Kiyahudi walianza kutafuta njia ya kumwua Yesu.



ulimwengu. Waliona uchungu wakati maadui zao walipotubu na kupata kibali mbele zake.

**SEHEMU YA TATU: Malaki**

Malaki alikuwa nabii wa mwisho kati ya manabii wale ambao Mungu aliwainua ili waonye watu wake wateule. Malaki alikuwa akiishi miaka 400 kabla ya kuzaliwa kwake Yesu. Tena katika kitabu cha Malaki tunaambiwa ya kuwa watu walio wateule wa Mungu wameanza kumtia uchungu tena. Wana wa Israeli hawakuweza kulifahamu kusudi la Mungu katika kuwatumia kuwaongoza watu wa Mataifa kumwamini Mungu.

Malaki 1:10-11 ni onyo kali kwa wana wa Israeli kwamba watubu, au watapata hukumu ya Mungu wakiwa kama taifa. Malaki ameonya kuwa Mungu atawachagua watu wa taifa lingine ili litimize kusudi lake, kwa sababu kusudi la Mungu la kumpatanisha mwanadamu naye litatimizwa.

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Agano la Kale limefunga kwa kutoa onyo na kuwaita wana wa Israeli watubu. Ni jambo la kuhuzunisha kwamba kwa muda wa miaka elfu nyingi tangu Ibrahimu kupokea ahadi hii na tangu taifa kuundwa chini ya uongozi wa Musa, wana wa Israeli walikuwa bado hawajafahamu kusudi la Mungu katika maisha ya taifa. Miaka mia nne baadaye Mungu mwenyewe akiwa nafsi ya Yesu aliita mwito wa mwisho wa kufikia kwenye toba.

## Mpango wa Sita

# AHADI ZA MUNGU ZIKITIMIZWA NA YESU

**Kiini cha Mwezi:** Ujumbe wa Kueneza Injili

**Maandiko ya Ibada Fupi:** Yeremia 31:31-34

**Kifungu cha Kukumbuka:**

"Angalia, siku zinakuja, asema Bwana, nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda."

Yeremia 31:31

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Yesu alipozaliwa, ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu ilitimizwa. Mungu alikuwa amemwahidi Ibrahimu kuwa katika uzao wake watu wote wa dunia watabarikiwa. Luka na Mathayo wameandika orodha ya majina yanayoonyesha kwamba Yesu alikuwa wa uzao wa Ibrahimu. Yesu alipozaliwa, malaika waliwaambia wachungaji kuwa Yesu ataleta amani ulimwenguni kwa watu wote aliowaridhia.

**SEHEMU YA KWANZA:** Ahadi ya Kale

Wana wa Israeli walishindwa kuushirikia ujumbe wa Mungu kwa watu wote wa dunia kama vile alivyokuwa amekusudia. Mungu alikuwa mstahimilivu sana kwa wana wa Israeli. Alikuwa amekwisha wapa nafasi nyingi ili wawaambie watu wa ulimwengu habari za pendo lake na kumsaidia mwanadamu kuishi akishirikiana na Mungu. Sasa Mungu alikuwa akimtumia mmoja wa uzao wa Ibrahimu katika kuibariki dunia nzima.

Maisha ya Yesu ni maisha ya Mwana wa Mungu akiwa kati ya watu. Katika maisha ya Yesu, Mungu anapeleka pendo lake nje ya mipaka ya taifa la Israeli.

**SEHEMU YA PILI:** Ahadi Mpya

Mungu alipomtuma Mwanawe hapa ulimwenguni, alifanya ahadi mpya na watu wake. Sasa Israeli siyo taifa la Mungu. Wateule wa Mungu watakuwa watu wale wote wanaompokea Yesu kuwa Mwokozi na kuanza kutembea wakishirikiana naye.

Watoto wa ahadi mpya watakuwa wale ambao amri za Mungu zimeandikwa katika mioyo yao. Warumi 9:8 husema ya kuwa "...si watoto wa mwili walio watoto wa Mungu, bali watoto wa ile ahadi wanahesabiwa kuwa wazao."

**SEHEMU YA TATU:** Yesu, Mwokozi wa Ulimwengu

Katika Mathayo 13 Yesu anasema ya kuwa ufalme wa mbinguni unafanana na punje ya haradali au chachu katika mkate. Katika mahubiri yake juu ya mlima yanayopatikana katika Mathayo 5, Yesu aliwaambia wanafunzi wake ya kuwa wao ni kama chumvi na nuru ya ulimwengu. Maneno haya yanaeleza vile ufalme wa Mungu unapaswa kuenea kote ulimwenguni. Mwanzo wa ufalme utakuwa mdogo, lakini mwishowe utaenea na kufunika ulimwengu mzima. Injili ya Yesu Kristo ni nuru kwa ulimwengu wenye giza.

Kazi ya Yesu ya kuhubiri hapa ulimwenguni ilikuwa kwa muda wa miaka mitatu. Muda wa miaka hiyo mitatu, alilifundisha na kulijenga kundi ndogo la wanafunzi jinsi ya kuweza kuieneza Injili kwa watu wote wa ulimwengu.

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Ahadi ya kale iliwategemea wana wa Israeli jinsi wangaliweza kuzitii amri zake alizompa Musa. Zile amri kumi ziliandikwa juu ya bao za mawe. Naye ahadi mpya ya Mungu inasema ya kuwa ataishi ndani ya mioyo yao. Mara tu Yesu aingiapo ndani ya moyo wa mtu, ahadi mpya ya Mungu huwa imetimizwa.



## Mpango wa Saba

# YESU NA WAYAHUDI

**Kiini cha Mwezi:** Ujumbe wa Kueneza Injili Katika Biblia

**Kifungu cha Ibada Fupi:** Luka 4:16-30

**Kifungu cha Kukumbuka:**

"Kwa maana Kristo ni mwisho wa sheria, ili kila aaminiye ahesabiwe haki."

Warumi 10:4

**KIONGOZI WA MPANGO:**

Yesu alianza kuhubiri na kuwatuma wanafunzi wake kwenda kwanza kwa wana wa Israeli. Wana wa Israeli walipewa nafasi nyingine tena ili watubu hali yao ya kumwasi Mungu, wamwamini, na wamtii yeye kisha watimize ahadi yake. Kwanza Yesu alistaajabu kwa sababu wana wa Israeli walikataa kumwamini. Hatimaye aliweza kufahamu ugumu wa mioyo yao. Aliweza kuona vile wana wa Israeli walivyomchukia Mungu ingawa walikuwa wakifikiria kuwa wao ndio waliokuwa wakimwabudu Mungu wa kweli.

**SEHEMU YA KWANZA:** Msamaria Mwema

(Soma Kutoka Biblia Yako: Luka 10:25-37). Katika Injili ya Luka 10 Yesu anasimulia habari za hadithi ya Msamaria mwema. Yesu alisema ya kuwa amri za Mungu huamuru kila mmoja wetu ampende jirani yake kama vile anavyojipenda nafsi zake. Hadithi ya Msamaria mwema hutuambia ya kuwa mtu ye yote mwenye shida ni jirani yetu. Katika hadithi hii watu wale wa dini